

KUUPIGANIA ULE URITHI KATIKA NCHI YA AHADI

Kumbukumbu ya Torati 1:6 – 8

“Bwana, Mungu wetu, alituambia huko horebu, akasema mliyokaa katika mlima huu vyatosha, geukeni mshike safari yenu Angalieni, nimewawekea nchi mbele yenu, ingieni mkaimiliki nchi BWANA aliyowaapia baba zenu, Ibrahimu na Isaka, na Yakobo, kwamba atawapa na uzao wao baada yao”

Ni wangapi waliosoma nyuma pale katika kumbukumbu 1 pale, ambapo wapelelezi walienda hasa pale na kuonja vitu kutoka Kanaani, ambapo Kanaani siyo mfano wa miaka elfu. Wangapi wanajua hilo? Kanaani siyo mfano wa utawala wa miaka elfu, kwa sababu walikuwa na vita, mapigano, mauaji, na kila kitu katika kanaani, Kanaani ni mfano wa Roho Mtakatifu. Misri ni dunia ambayo wametoka katika hiyo. Kule Jangwani ndiyo mahali walipotakaswa na wakaitwa Kanisa. Kanaani ni walipopumzika wakiwa na Roho Mtakatifu. Kwa sababu walikuwa bado na vita. Na kama huamini ya kuwa una vita, mpate Roho Mtakatifu mara moja uone.

Unafanya nini? Wanafanya nini ndani ya Kanaani? Walikuwa wanamiliki haki zao. Utukufu, Walikuwa wanamiliki haki zao. Na wasingeweza kumiliki ahadi zao mpaka wameingia Kanaani. Hawakuwa na chochote cha kwao huko jangwani. Halafu, walipofika Kanaani, hapo sasa walikuwa na haki. Na sisi tunazo haki. Unapompokea Roho Mtakatifu, uko Kanaani. Inabidi ulipigania hilo, kila inchi moja ya aridhi, inabidi uipigania. Ndiyo, Bwana. Hiyo ndiyo sababu watu wanasema, “Ndugu Branham, niombe mimi leo, mimi” unaona? Ingia Kanaani mara moja ndugu na utatambua wewe ni wa wapi. Angalia maombi yanavyo anzisha mambo ng’ambo kule sasa. Ndiyo, Bwana.

Alisema, “angalia hapa, Shetani. Hii ni yangu. Mimi ni mmiliki wa hii. Mungu amesema hivyo. Toka (Hiyo ni sawa) Ondoka kwenye aridhi yangu”

“Eneo lako?” Shetani anasema. “Ninayo hati miliki ya hiyo, Toka uende. Unajua. Nitakuandikia onyo kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, Inabidi aondoke aende. Hakika ni lazima afanye hivyo.

Sasa, kumbuka, aliwapa wao ile nchi, lakini ilibidi wapigania kila inchi yake. Mungu alimuambia Joshua, Popote pale unyayo wa mguu wako utakapokanyaga, hapo nimekupa wewe” Unyayo wa mguu ulimaanisha umiliki (2Kor. 10:3 – 6). Tunawafukuza tupa chini, na kuchukua lile Neno. Chukuwa neno, uendelee. Neno linasema hivyo.

Sasa, unasema, “Kwa hiyo ahadi ni yangu” Ndiyo lakini utaipigania kila inchi yake mpaka uwe mzima. Inakupasa uchukue kila hatua ya hilo. Ni vita. Ahadi ni yako. Hiyo ni nchi iliyo ahidiwa, ilibidi wapigania kila hatua waliyoichukua. Na ahadi ni yako, lakini utapigania kila inchi yake.

Ndugu Branham aliendelea kusema: Nimeitwa na Mungu kuhubiri Injili miaka thelathini na moja iliyopita. Nimepigana tangu wakati huo. Kila inchi ya aridhi imenilazimu kupigana kwa upanga wa Mungu, kuichukua ahadi, na kukatakata kupata njia.

Mungu alitoa ahadi tukaeni nayo. Mungu aliahidi. Haijalishi.... Lazima uwe na vita. Kama kila kitu kinakuja kirahisi, utakuwa unashinda nini? Walishinda kwa Neno la Mungu na ushuhuda wao, kwa damu ya Kristo (ufunuo 12:11). Lazima ushinde jambo fulani, na ni lazima upate vikwazo. Na watu wanaopishana/tofautiana nawe, na kushindana nawe, na kukuambia wewe ni mtakatifu anayevingirika na mambo yanayowekwa mbele yako, ili kukujaribu. Kama huna hayo, basi hata huko vitani.

Kwa nini umejiunga na Jeshi na kupata mafunzo? Ili kulala tu, kutembea kwa madaha mitaani na kujionyesha? Hivyo ndivyo wakristo wengine wanavyofanya, kwamba tunataka tuangaliwe. Hutaenda kuangaliwa tu. Utaenda kudharauliwa/kuudhiwa. Wote wapendao kuishi maisha ya utawa katika Kristo Yesu wataudhiwa (2Timo 3:12). Chukua upanga.

Joshua na Kaleb, waliwanyamazisha watu. Watu walisema” hatuwezi kuichukua”, hatuwezi kufanya hivyo. Hakika “Unaona, walikuwa wanawaangalia Waameleki. Joshua na Kaleb walikuwa wanaangalia ahadi. Hiyo ndiyo tofauti. Inategemea unaangalia nini (Hesabu 13:26 – 33).

Joshua alisema, “Sisi ni zaidi ya washindi. Tu zaidi ya washindi. Kwanini? Alisema “wao ni chakula kwetu. Kwa nini, wanaonekana wakubwa. Wanaonekana wakubwa. Lakini tutakuwa na mkate mkubwa” alisema, Mungu ametupa sisi ahadi, na hofu yetu iko juu ya kila mmoja. Ingawa bado wanatofautiana nasi, bado wanatuogopa sisi” Hakika. Alisema, “Hofu ya Mungu iko juu ya kila mmoja wao. Wanaogopa kiasi cha kufa “alisema, twende tukaitwae hiyo. Mungu ametupa hiyo, kwa hiyo ni yetu. Tusonge mbele na tuichukue (Hesabu 14:1 – 10)

Vema, Je uliona muda mfupi tu kabla ya kufika nchi ya ahadi, kabla hawajaingia katika nchi ya ahadi, ambayo ilikuwa ni umbali wa siku chache tu, siku kumi au kumi na moja, pengine sio kiasi hicho, kwa sababu ilikuwa ni kama maili arobaini au kitu kama hivyo. Walikuwa waingie katika nchi ya ahadi, walipita hatua zote za safari walikotembea. Walivuka bahari ya Shamu, majeshi ya Farao yakazama nyuma yao. Walikuwa huru na maadui zao, waliendelea kupitia jangwani, na wakafika mpakani mwa nchi ya ahadi pale Kadesh Banea, na pale walishindwa (Hesabu 13+14) kwa nini? Kwa nini walishindwa?

Sasa, Musa aliyaambia yale makabila kumi na mbili alisema, “Atamtuma mtu kutoka kila kabila ili kuwakilisha kila kabila, kwenda kupeleleza ile nchi kuona iko katika hali gani”

Sasa, hapo ndipo hasa mahali, ambapo unapitia / umefikia. Kanisa limepitia kuhesabiwa haki kwa Imani, kupitia utakaso kwa Wamethodist, na sasa ni wakati wa ahadi. Ahadi ni ubatizo wa Roho, ambao umeahidiwa wote kupitia Agano la Kale na jipya pia, ile ahadi “Tazama, nawaletae juu yenu ahadi ya Baba yangu.....”(Luka 24:48 – 49). Petro alisema hayo siku ya pentecoste.

Hiyo ni ahadi. Nchi ya ahadi ni kuishi katika nchi ya Roho Mtakatifu. Ni nchi nyingine. Inabidi utoke kwenye mazingira/hali ulizokuwa nazo, kutoka ili kuishi katika nchi hii ya ahadi ili upokee ahadi. Kumbuka ahadi, “Mtapokea nguvu kutoka juu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu”(Matendo 1:8).

Na Petro alisema ile ahadi iliyotolewa tangu nyuma Agano, la kale na Jipya..... Unaona hiyo ahadi, inakuja mpaka siku ile ya Pentekoste, na hapo sasa wakaingia kwenye ile ahadi.

Kumbuka, Joshua na Kaleb walikuwa wawili pekee katika lile kundi lote la watu milioni mbili na nusu waliovuka kuingia katika nchi ya ahadi. Kwa sababu walienda kuingia nchi ya ahadi, na wakapata baraka, na kurudia na kusema, “Tunao uwezo wa kuitwaa, kwa sababu Mungu amesema hivyo”.

Na hapo walisimamia. Kwa nini? Sasa, watu hao wote waliangalia mazingira, lakini Joshua na Kaleb walikuwa wanaangalia kile Mungu alichosema. “Nimewapa ninyi ile nchi, nendeni mkaitamalaki/mkaichukue”.

Mkristo halisi anapigania nafasi yake. Inabidi asimame peke yake, Yeye na Mungu, naye anapigania kila inchi ya sehemu / ardhi, kwa hiyo huhitaji kuwabembeleza hapa na pale.

Lakini sasa, na tukiendelea. Je uliweza kuona hili, Musa yule aliyetenda miujiza ile mikuu ambaye aliwaleta Israel kupita nchi hizo zote, na kuwaleta mpaka kuifikia nchi ya ahadi, lakini hakuweza kuwapa urithi wao? Hakuwapa urithi wao, aliwangoza wao kwenye nchi, lakini Joshua aliigawanya nchi kwa watu. Hiyo ni kweli? Na Kristo alilileta Kanisa mpaka mahali ambapo urithi wao ulikuwa umeshatengenezwa, wameshapewa, ilikuwa tu wavuke Yordani, lakini Roho Mtakatifu, ndiye anayeliweka Kanisa katika utaratibu, Joshua wa leo analiweka Kanisa katika utaratibu, akimpa kila mmoja, karama, mahali, nafasi. Na Yeye ni sauti ya Mungu ikizungumza na mtu wa ndani ambaye Kristo amemuokoa: Roho Mtakatifu.

Sasa, kwa kiasi hicho unalipata hilo? Sasa, tunaenda katika kitabu cha Waefeso. Sasa, kwa njia ile ile, Analilweka Kanisa mahali pake. Sasa, Joshua aliwaweka katika nchi ya asili dunia. Sasa Roho Mtakatifu analiweka Kanisa mahali pake, katika mahali ambapo linakaa, urithi wao.

Sasa, ili darasa lisisahau, tunaingiaje ndani ya Kristo? Tunajiunga na Kanisa ili tuwe ndani ya Kristo? Je tunakiri ili tuwe ndani ya Kristo? Tunazamishwa katika maji ili kuwa ndani ya Kristo? Tunaingiaje ndani ya Kristo? (1kor. 12) Kwa Roho mmoja (Roho mkuu, ambaye ni Roho Mtakatifu) tumebatizwa sote ndani ya nchi ya ahadi” (1kor. 12:13).

Katika nchi hii ya ahadi, kila kitu ni chetu katika nchi hii ya ahadi.

Waisraeli walipovuka Yordani kuingia nchi ya ahadi, walipiga na kuangusha chini kila kitu.....

Sasa, kumbuka, katika nchi hii ya ahadi, haimaanishi kwamba wewe hutaugua; haimaanishi kwamba hutapata taabu. Lakini inatamka hivyo (oh, hebu hili lizame ndani); inasema hivi, kwamba ni yako. Inuka tu na uichukue.

Tunapokuwa ndani ya Kristo, tunakuwa na baraka za rohani. Nje ya Kristo tunakuwa na misisimko. Ndani ya Kristo tunazo baraka halisi, siyo za kujifanya, siyo za kuigiza, sio za kujibandikiza. Lakini ili mradi unasema uko kwenye nchi ya ahadi, na hauko, dhambi zako zitakudhihirisha. Na jambo la kwanza unajua, utajikuta mwenyewe umetatanika na vyote, kama tuitavyo katika dunia, umezingirwa. Utatambua kwamba hunacho kile unachokizungumzia. Lakini unapokuwa ndani ya Yestu Kristo, Amekuahidi amani ya Mbinguni, baraka za kimbinguni, Roho wa kimbinguni, kila kitu ni chako. Uko kwenye nchi ya ahadi na ukiwa unamiliki kikamilifu kila kitu. Amen. Jinsi ilivyo yakupendeza. Oh, hebu tujifunze hilo.

Sasa, hapo ndipo ambapo Kanisa linatatizika/kukwazika vibaya.”Sawa ona alivyotuchagua sisi ndani yake.....” Nani? Kristo (Waef. 1:3 – 7). Tunalipataje hilo? Tunajuaje hilo? Mungu kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu alitukusudia sisi. Nani? Wale walioko kwenye nchi ya ahadi.

“.....alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo.... Sawa sawa na uradhi wa mapenzi yake, kwa sifa ya utukufu wake..... (kwamba tuweze kumsifu kama alivyosema. Hivyo ndivyo alivyo, Mungu, tunataka kumsifu yeye)....usifiwe utukufu wa Neema yake ambayo umetufanya tukubaliwe kwa huyo mpendwa ndani ya Kristo tumekubaliwa). “Ambaye katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi....”

Sasa, kumbuka, Mungu alikuchagua wewe kwa ufahamu wake wa mbele, kwamba ulikuwa unakuja katika hili. Mungu kwa ufahamu wake wa mbele, alikuchagua wewe kuja katika nchi ya ahadi. Ni nini nchi ya ahadi kwa Mkristo leo? Ile ahadi ni kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa wote walio mbali (Matendo 2:39). Na katika Isaya 28:18, Amri lazima iwe juu ya amri, mstari juu ya mstari, hapa kidogo, na hapa kidogo, shikilia kwa nguvu lile lililojema. La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa, ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu (hii ni raha) nchi ya sabato ambayo nilisema wataingia ndani yake. Na

lakini hawakutaka kusikia, wakatikisa vichwa vyao, na kwenda zao wala hawakutaka kusikia” Unaona? Sahihi.

Angalia hapa katika Waebrania 4:1 – 10, je hakuzungumza kuhusu pumziko lingine? Mungu aliiumba siku ya saba na akawapa wao pumziko siku ya saba (Mwanzo 2:1 – 3). Mahali pengine alizungumzia pumziko akisema, “leo katika Daudi”. Hapo tena aliwapa pumziko lingine, “njooni kwangu mnaosumbuka na kulemewa na mizigo nami nitawapumzisha”.

Ingia katika hili pumziko (Matayo 11:28 – 30). Kwa maana sisi tulioingia katika hili pumziko, tumekoma kufanya kazi zetu kama Mungu alivyofanya katika siku ya sabato. Kwa hakika. Hiyo ndiyo sabato yako, pumziko. Hapo sasa hilo ndilo pumziko halisi katika nchi hii ya ahadi.

Unaona hilo? Kule kuingia katika nchi hii ya ahadi. Tunaingiaje? Tumechaguliwa kimbele katika hilo, Kanisa, kwa ufahamu wa kimbele wa Mungu. Tumechaguliwa kimbele kwa ajili gani? Kwa ajili ya utukufu wake, kwa neema yeke, kwa utukufu na Ibada na utukufu wa Mungu. Baba, akiwa amekaa nyuma pale mwanzo, yeye aishiye pekee, hakuna chochote kinachomzunguka Yeye, alitaka kitu fulani cha kumwabudu, kwa hiyo alitangulia kukusudia na kuchagua kimbele Kanisa, na kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na akaweka majina yao katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, kuwa waweze kuonekana kwa utukufu wake na sifa zake katika siku za mwisho, atakapovikusanya vitu vyote ndani ya mtu mmoja, Kristo Yesu. Ooh. Utukufu. Hilo hasa. Na hilo ni sawasawa. Ndugu yangu na dada. Kamwe usisogee kamwe katika hilo.

Ni kitu gani kinawafanya wasiwe wa kawaida? Ninyi ni Taifa takatifu (1Petro 2:9 – 10). Umeifanya nini? Umeingia kutoka nchi ile. Uko kwenye nchi nyingine. Umewezaje kufika pale? Ile ni nchi ya ahadi. Ni ahadi ya namna gani? “Na itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu”, (Matendo 2:14 – 18). Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika nchi hii moja ya ahadi. Amen. Kaka zangu na dada (Halleluya). Kwa usafi wote wa moyo, hakuna wivu, hakuna uadui, hakuna Sijali kama ndugu ataenda pembeni, haijalishi anafanya nini, utaenda kwa ajili yake.

Nilimuendea ndugu mmoja aliyepotoka siyo muda mrefu uliopita. Kijana mdogo aliniambia mimi, “Muache huyo mtu mbaya aende. Muache peke yake. “Nikasema,” Kama nitafikia mahali ambapo moyo wangu hautaweza kumuendea ndugu, hapo sasa ni wakati wa mimi kwenda madhabahuni, kwa sababu nitakuwa nimeanguka kutoka kwenye neema”. Nilisema, “nitamuendea ili mradi anayopumzi katika mwili wake, na nitampata mahali fulani katika mstari”. Ndiyo bwana nami nilimpata (Halleluya), nikamrudisha tena. Ndiyo Bwana. Yuko kwenye zizi akiwa salama sasa. Ndiyo, Bwana. Angeenda njia mbaya kwa uhakika kama dunia ilivyo. Kwa maana Petro alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, na mbatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu

(nchi ya ahadi iliyoahidiwa), na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjije”.

Kulitokea nini (katika Hesabu 13 na 14)? Nawauliza ninyi sasa, mimi ni mlinganishaji, na mtu yoyote anayejua Biblia ni mlinganishaji. Je yupo hata mmoja wa hawa watu walioiona ile nchi ya ahadi? Hakuna hata mmoja. Nani walifanikiwa? Nani walivuka kwenda kule? Ni wale walioenda kwanza, wakaja, na kusema, “Tunaweza kuichukua hiyo. “Tunaweza kumpata Roho Mtakatifu kwa sababu Mungu alisema hivyo”.

“Petro alisema siku ya Pentekoste, kama nitatubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, Nitampokea Roho Mtakatifu, ahadi hii ni kwa ajili yangu. Niko tayari kufanya hivyo, ni yangu. “Unalipata hilo? Sasa, ahadi hiyo yangu. Ninaipokea, ni yangu. Hakika ni yangu. Walikuwa ndio hao pekee (matendo 2:38 – 41)

Wao ni kama wana wa Israel ambao walitoka Misri na kusimama wakiwa hawajafika nchi ya ahadi. Sasa hawa wana wa Israeli waliondoka Misri kiasi cha milioni mbili wenye nguvu. Wote walisafiri pamoja, wote waliona miujiza ile ile ya Mungu, wote walishiriki ile mana na maji yaliyotoka kwenye mwamba uliopigwa, wote walifuata wingu lililele mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku, lakini ni wawili tu ambao walifika Nchi ya Ahadi. Wawili tu ndio waliokuwa wakweli au waaminio halisi. Hiyo ni sawa kwa sababu neno linatuambia kwamba wengineo wote walikufa kwa sababu ya kutokuamini, na kwa sababu ya kutokuamini hawakuweza kuingia (Waebr. 3:19). Kwa sababu hiyo ni kweli, na ni wawili tu walioingia, basi waliobakia wote hawakuwa waaminio wa kweli. Ni kitu gani kilifanya tofauti? Wawili walikaa na Neno. Wakati mioyo ya wale wapelelezi kumi iliposhindwa pale Kadeshi Benea, Joshua na Kaleb hawakusita kwa sababu waliamini kile Neno limesema, “Twaweza kushinda bila shaka kuichukuwa hiyo nchi” Walijua wanaweza kwa sababu Mungu amesema, Nimewapa ninyi hiyo nchi”. Pamoja na haya yote Waisraeli hawa waliona nguvu na uzuri na ukombozi wa Mungu na bado hawakuweza kuingia kwenye pumziko, ambalo ni mfano wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo unaweza kuona sasa kuwa ni wachache sana watakao amini njia yote mpaka kumpokea Roho wa Mungu.

Sasa, natusimame kama Joshua na Kaleb. Nchi yetu ya ahadi inaanza kuonekana kama ile ya kwao. Sasa Joshua maana yake ni “Jehova – mwokozi”, naye anamuwakilisha yule kiongozi wa wakati wa mwisho ambaye atakuja kwa ajili ya Kanisa kama vile Paulo alivyokuja kama kiongozi wa Mwanzo. Kaleb anawawakilisha wale waliokuwa wamesimama kwa uaminifu na Joshua. Kumbuka, Mungu alianza na Israeli wakiwa ni bikira wa neno lake. Lakini walitaka kitu fulani tofauti. Kadhalika ndivyo lilivyofanya Kanisa la wakati wa mwisho. Angalia jinsi ambavyo Mungu hakuwasogeza Israeli, au kuwaacha waingie katika nchi ya ahadi mpaka wakati wake mwenyewe alioukusudia. Sasa inawezekana watu walimuwekea Joshua msukumo, yule kiongozi na kusema, “Nchi ni yetu, na twende tukaitamalaki. Joshua, inaonekana umekwisha, utakuwa umepoteza agizo lako, huna nguvu kama ulizozoea kuwa nazo. Ulikuwa umezoea kusikia kutoka kwa Mungu na kujua

mapenzi ya Mungu, na kutenda haraka; “Kuna kasoro fulani uliyonayo”. Lakini Joshua alikuwa ni Nabii aliyetumwa na Mungu. Naye alijua ahadi za mungu, kwa hiyo alizingojea. Alingojea agizo la wazi na la mkato kutoka kwa Mungu na wakati wa kuondoka/kusafiri, ulipofika, Mungu aliuweka uongozi mkamilifu mikononi mwa Joshua kwa sababu alikaa na Neno. Mungu alimwamini Joshua lakini sio hawa wengine kwa hiyo itajirudia tena katika wakati wa mwisho. Tatizo lilelile na msukumo uleule.

Kukusudiwa kimbele kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili hufanywa wana, kukusudiwa kimbele kwa uzima wa milele. Sasa, baada ya kuja katika uzima wa milele, baada ya kuokolewa, kutakaswa, na kujazwa na Roho Mtakatifu, Ninyi ni wana. Sasa, Mungu anataka akuweke mahali pako, oh, ili uweze kutenda kazi kwa ufalme wake na kwa utukufu wake.

Hiyo ni Injili. Ukiwa kwanza, umesikia Neno, “Tubuni, makabatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi” kuondoa kabisa dhambi zako zote, uliite jina la Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya nchi ya ahadi.....ile ahadi ni kwa ajili ya wasafiri wote walio njiani. Kama umeacha nyumba yako usiku wa leo, mwenye dhambi, ukisema “Nitaenda kule maskanini, Mungu anakupa nafasi usiku wa leo, kuna kitu kimoja kinasimama kati yako na nchi ya ahadi Ni nini nchi ya ahadi? Roho Mtakatifu kulikuwa na kitu kati ya Yoshua na nchi ya ahadi ni Yordani. Ndivyo hasa.

Musa akiwa ni mfano wa Kristo, aliwaongoza watoto mpaka inchi ya ahadi; halafu Musa hakuwachukuwa watoto katika nchi ya ahadi. Yoshua aliwachukuwa watu na kuwagawia nchi ile. Yesu alilipa deni/gharama, akawaongoza kwenye Roho Mtakatifu. Mungu akampeleka Roho Mtakatifu, chini, na akaliweka Kanisa mahali pake kwenye utaratibu, kila mtu akimjaza na uwepo wa utu wake unaona ninachomaanisha? Vyote ndani ya Yesu Kristo, jinsi Mungu alivyokusudia hili kimbele kuitwa kwa Injili hii.

Paulo, Wagalatia 1:8, alisema, “Kama Malaika atahubiri kitu kingine tofauti, na alaaniiwe” ule ukweli, ile Injili.....sasa, sikiliza kwa karibu tunaposoma, kumalizia mstari.

Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia Neno la kweli, habari njema za wokovu, wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu (Waefeso 1:13).

Na kumbuka, dhambi waisraeli waliyoifanya (kwa Balaam kuwaambia sisi wote ni sawa), dhambi ile kamwe Israeli hawakusamehewa (Hesabu 25:1-9) Na angalia; Ngoja nikupe hesabu ya kushangaza; kati ya milioni mbili waliotoka Misri, wawili tu waliingia nchi ya ahadi kila mmoja wao alikula chakula kile kile; wote walicheza katika Roho; walikuwa wote wana vitu shirika. Lakini ulipokuja wakati wa kutenganishwa, Lile Neno lilitenganisha. Hivyo hivyo hata leo Neno lilifanyakazi ya kutenganisha. Ulipokuja wakati alisema, “kwa nini tupo hapa.....”

Waisraeli wote, baada ya kumuona Musa akitenda na kuwaleta juu mpaka kwenye baraza kuu, ambapo mkutano ulifanywa kila mmoja alisema, “vema nenda na Balaam, kwa sababu tunafikiri, Daktari Balaam yuko sahihi. Ni mjanja, ana Elimu, kila kitu, kwa hiyo tutachukuwa hilo”

Na Mungu kamwe hakuwasamehe hao. Aliwaangamiza kulekule jangwani. Na Yesu alisema mwenyewe” Hawatakuwepo’ hakuna hata aliyeokolewa”

Walisema, “Baba zetu waliila mana jangwani kwa miaka arobaini” Alisema, “kila mmoja wao amekufa (kutengwa milele na Mungu) kila mmoja wao amekufa”. Kwa hakika kwa sababu walisikiliza makosa wakati Musa akiwa amethibitishwa na Mungu na kiongozi wa kuwaonyesha wao njia ya kuelekea nchi ya ahadi, na wamefikia umbali huo sawa, lakini hata hivyo hawakuweza kwenda pamoja naye.

Sasa, waaminio wanaweza kuliona hilo, lakini wasioamini hawawezi kuliona hilo likithibitishwa.

Kama vile Musa alivyoita taifa kutoka ndani ya taifa, Kristo leo anaita kanisa kutoka ndani ya kanisa, jambo hilo hilo kwa ulinganifu, kuwachukua kwenye nchi ya ahadi ya utukufu ya milele. Lakini hapa anakuja Musa, mtumishi mwaminifu ambaye alihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina zote za Misri (Waebr 11:23-27) alifikia mwisho wa safari, akiwa mtu mzee, miaka mia na ishirini, alitembea juu mlimani na alijua kwamba kifo kiko mbele zake, na aliitazama nchi ya ahadi (Kumbukumbu 34) naye akaiona, ikiwa iko ubavuni pake, kiongozi wake akiwa pale, ule mwamba. Alirukia mwamba na malaika wa Bwana wakamchukua kumpeleka utukufu utukufu wa Mungu, katika kifua cha Mungu kwa nini? Miaka mianane baadaye, alikuwa bado anaongozwa na kiongozi wake (Mt. Matayo 17:1-8).

Na Mungu kamwe hakuweza kushughulika na waisraeli mpaka wamerudi katika nchi yao. Nisikieni mimi HII ASEMA BWANA, Mungu hatashughulika na Kanisa lake mpaka limekuja katika nchi ya nyumbani/ahadi, ujumbe wa saa hii. Njooni kwenye kile cha mwanzo. Achaneni na mawazo yenu ya Kimethodist, Kibaptist, kipresbyterian, upentekoste wenu, uassemblies, umoja, utatu, kanisa la Kristo vyote hivyo ni vyama vya Mpinga Kristo nami najua haya yanaenda ulimwenguni kote. Yote yako makosani, yote ni ya shetani.....kuna watu wa Mungu ndani ya kila moja, watu wa Mungu ndani ya hayo yote, lakini utaratibu wenyewe sio wa Mungu na Mungu kamwe hataubariki. Hajafanya hivyo kamwe.

Haijalishi umekuwa Mkristo kwa muda mrefu kiasi gani. Je unazo hizi roho za zamani duni ambazo zinazungumza na wewe, zinakufanya unakuwa mwenye hasira, zinakufanya uzungumze juu ya mtu mwingine? Wakati mtu akija na kuanza kuzungumza juu ya mtu mwingine, unaangana haraka nao na oh, na kuanza msululu wa kuwasema? Hiyo siyo sahihi ndugu; usifanye hivyo. Hili litakuzuia hatimaye usiende katika nchi ya ahadi. Kama unavyo vitu hivi vidogo vya zamani ambavyo hupaswi kuwa navyo, kama upendo wa Mungu hauko hasa moyoni

mwako, je si uje hapa na kusema, “Mungu, hapa hapa ninaenda kuumwaga kule. Yote hapa hapa. Ninaondoka hapa madhabahuni nikiwa mtu tofauti “Je utakuja?

Nukuu za Kiingereza

“Maswali na majibu” (59 – 1223), Kitabu cha COD uk 508 Swali na 106 “Presuming” (kufanya pasipo ruhusa) (62 – 0408), Aya 32 – 39. “Maswali na majibu” (61 – 10515M), Kitabu cha COD uk 659 – 660, Swali na 152. “Wana wa Mungu waliodhihirishwa” (Kufanywa wana sehemu II) Aya 19, 31 – 36, 103, 124, 129,132,140, - 142, 196. “Nafasi ndani ya Kristo” (kufanywa wana sehemu II), Aya 189,202, Kung’ang’ania (kitabu 19 na 9) Aya 94; “wakati wa Kanisa la Simirna” CAB uk. 148. “Wakati wa Kanisa Pergamo” Kitabu cha Nyakati saba uk. 172. “Kufanywa wana” (kufanywa wana sehemu 4), Aya 112 – 114. “Matukio ya leo yakiwekwa wazi na unabii” (kitabu 7 na 6), Aya 124, 178 – 182. “Uongozi” (kitabu 7 na 7) Aya 141, 279/ “Maelekezo ya Gabriel kwa Daniel” Aya 133. “Watoto kule jangwani” (47 – 1123), Aya E – 28/ “Roho zinazodanganya” (55 – 0724), Aya 135.

jiwe la kiroho la kujengea na 104 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kenju,
Box 5138, Tanga
E-mail: chaelika@hotmail.com
Cell.phone 0784704299*